

Unatakiwa Kufanya Nini?

Tafadhali andika majibu yako kwa kila swali kwenye nafasi uliyopewa. Kumbuka kwamba hakuna majibu yasiyokuwa sahihi. Tafadhali tafakari kwa makini kuhusu maswali hayo na utoe maoni yako mwenyewe.

KISA CHA 1

Samira na rafiki yake mkubwa Yonah wamezozana sana. Baadaye, Samira alisambaza chapisho baya sana kumhusu Yonah kwenye mitandao ya kijamii. Baadaye usiku huo, Yonah anamtumia ujumbe wa maandishi na wanasameheana, lakini chapisho lake bado lipo mtandaoni.



Ni nini kinachoweza kutokea? _____



Samira afanye nini? Yonah afanye nini? _____



Je, unaweza kufikiria mfano halisi wa maisha wa kisa kama hiki? _____



Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.

Unatakiwa Kufanya Nini?

KISA CHA 2

Hiwot aliwapiga picha baadhi ya marafiki zake wakifanya mambo ya upuuzi kisha akazichapisha kwenye mitandao ya kijamii, pamoja na alama za reli zinazoonekana kuwa za kifidhuli au zenye kudhalilisha, lakini ilikuwa ni katika hali ya utani kati yake na marafiki zake. Katika siku iliyofuata, Nyawira, rafiki yake mwingine, alikuja shuleni kwake na kusema alifikiri kwamba alama hizo za reli ziliumiza sana na zilionesha ubaguzi wa kijinsia (yaani, ubaguzi unaojikita katika jinsia, hasa ubaguzi dhidi ya wanawake).



Ni nini kinachoweza kutokea? _____



Hiwot afanye nini? Nyawira anaweza kufanya nini kingine? _____



Ingekuwaje kama Nyawira angekabiliana na Hiwot mtandaoni badala ya ana kwa ana? _____



Je, unaweza kufikiria mfano halisi wa maisha wa kisa kama hiki? _____



Ingekuwaje kama Nyawira angeanza kumwita mwonevu? Je, kuonwa kama mwonevu unadhani kunaweza kuathiri vipi sifa ya Hiwot katika siku zijazo? _____

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.

Unatakiwa Kufanya Nini?

KISA CHA 3

Abigail alikuwa kwenye mitandao ya kijamii alipogundua kwamba Selam, mvulana shuleni, amempiga picha na kuandika, "Haha #whatnottowear" (akiyakejeli mavazi yake). Bila shaka Abigail alikansirika sana.



Ni nini kinachoweza kutokea? _____



Je, Selam afanye nini? Je, Abigail afanye nini? _____

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.